**African Entrepreneurs – Successful and Responsible**

**Episode 5**

**Title: “A Business grows like a person” – Julian Omalla from Uganda**

**Author: Leylah Ndinda**

**Editors: Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch**

**Proofreading: Natalie Glanville-Wallis**

**Kisuaheli:Eric Ponda**

**Characters (O-töne, clips)/ Narrators**

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| Intro/Outro | | x | Unimportant | |
| Narrator | x | | Unimportant | |
| Julian Adyeri Omalla (clip) | x | | about 40 | English |
| Felix Omalla (clip) | | x | about 40-50 | English |
| Patricia Bilal (clip) | x | | about 30-40 | English |

**INTRO**

Hujambo na karibu kwa mara nyingi katika mfululizo wa makala ya ‘Learning By Ear’ Noa Bongo jenga maisha yako, tunapoendelea kuwangazia Wajarisimali Chipukizi Barani Africa ambao kwa juhudi na ufanisi wao wanaweza kuchangia kuboresha maisha miongoni mwa Jamii wanamoishi. Leo tunakutana na Julian Adyeri Omalla, Mfanyi biashara mashuhuri sana nchini Uganda. Mama huyu alihamia nchi humo kutoka Sudan ambako maisha ya umaskini yalikuwa jambo la kawaida. Lakini yote hayo sasa ameyapa kisogo baada ya kupata ufanisi mkubwa katika shughuli anazofanya. Kutokana na juhudi zake ameweza kubuni nafasi za kazi kwa zaidi ya watu 450 kutoka nchini Uganda na hata nchi jirani ya Sudan Kusini anakotoka. Tunakutana naye katika shamba lake lililoko mashariki mwa Uganda.

**0. SFX: Atmo (driving through) farm – to be recorded**

**1. Narrator**

Safari hii inatuchukua muda wa masaa manne kutoka mji mkuu wa Kampaka Uganda kufika katika shamba lake la ufugaji wa Kuku liliko Kidera Mashariki mwa Uganda.Ni shamba kubwa la linaloweza kutoshana na viwanja 200 vya mpira wa kandanda, na shughuli kubwa hapa ni kilimo cha mahindi. Kwa mpita njia utadhani shamba hili linatumika tu kwa kilimo cha mahindi na sio ufugaji wa kuku, kwani ilituchukua mwendo mrefu ndani ya shamba hili kabla ya kuona mabanda hayo ya Kuku.

## 2. SFX *:* Atmo... Chicken

## 3. Narrator

Katika shamba hili wafanyi kazi waliovalia sare za rangi ya samawati tayari wamaenza shughuli zao, na kila mmoja anaonekana akiifahamu vyema kazi yake, kwa kuzingatia ushirikiano uliopo bila ya kusimamiwa. Kuna wale wanaobeba chakula cha Kuku, wengine wanawapa kuku chakula huku wengine wakikusanya mayai. Kwa siku, shamba hili linauwezo wa kukusanya zaidi ya mayai 2000.

Kampuni hii inamilikiwa na Mama aliyeanza kazi hii kwa mtaji wa kiasi kidogo sana, lakini kutokana na uchu wake wa kutaka kupanua biashara hii, sasa amekuwa mfanyi biashara anayetambulikana kimataifa.. Jina lake ni Julian Adyeri Omalla. Unapokutana na Mama huyu mrefu na mnene, utadhani ni Mama mkatili. Lakini baada ya kutangamana naye kwa muda unatambua kuwa ni mama mkarimu na mcheshi sana.Julian mama wa watoto watatu na Bwanake afisa katika idara ya mahakama, alizaliwa miaka 44 iliyopita katika eneo la kusini Magharibi mwa Uganda, na akabahatika kusoma hadi shule ya sekondari.

## 4. Clip Julian 1

*Nimezaliwa katika familia maskini. Babangu alikuwa mwalimu na alikuwa na watoto wengi sanai.Mamangu alijaliwa kupata watoto saba lakini kuna watoto wengine walioishi katika familia yetu. Babangu alikuwa Mtu mkarimu sana. Alikuwa na watoto wengi wa kupanga kutoka kwa majirani jamaa na marafiki na kwa jumla tulikuwa familia ya kati ya watu 35 na 40. Kwa hivyo tuliishi katika hali ya usmakini, na nikiwa mdogo nilichukia sana kuishi maisha hayo ya umaskini*

## 5. Narrator

Juhudi zake za kupigana na umaskini zilimwezesha kuanzisha biashara yake katika eneo la mpakani kununua mahindi kutoka Kenya na Uganda kwa kiasi kidogo cha mtaji wa euro 100. Pia alinunua ngano na kuuza nchini Uganda. Lakini wakati washirika wake walipomtapeli akaamua kujitenga na kuanzisha biashara hiyo binafsi.

Kwa wakati huu Juliana Adyeri anamiliki jumla ya kampuni sita ikiwemo kampuni moja nchini Sudan Kusini. Anasema haogopi kufanya biashara yoyote ilmradi itamuletea mapato, na ndio sababu akachukua fursa hii kuanzisha biashara katika soko changa kabisa nchini Sudan Kusini licha ya muundo misingi duni nchini humo.Kampuni yake ya kwanza “Delight Uganda’ inayotengeneza kinywaji cha maji tamu ya “Cheers” aliianzisha mwaka wa 1996.

## 6. Clip Julian 2

*Mimi nilianza biashara hii kwa taabu sana. Nakumbuka nilikuwa nikisafiri hadi nchini Kenya kununua chupa. Kisha nikichemsha maji wakati wa usiku na kutengeneza Juisi asubuhi .Nilikuwa nikitumia toroli kuzungusha juisi hiyo mjini. Nakumbuka nilikuwa nikivalia rinda la rangi nyekundu na kuzunguka kila mahali sokoni nikiuza Juisi hiyo. Wakati huo sikuwa na pesa za kukodisha chumba cha biashara na nilitegemea kijibaraza cha rafiki yangu kuendesha biashara hii.*

## 7. Narrator

Kwa usaidizi wa wataalam wa kisayansi kutoka serikalini, Jualiana aliweza kuboresha bidhaa zake ambazo sasa zinauzwa kote nchini Uganda na hata nje ya Nchi.Hata hivyo lakini baadaye akaamua kugeukia ukulima na biashara ya mazao ya kilimo.

## 8. Narrator

Changamoto kubwa katika biashara yake ni kodi ya juu inayotozwa na serikali. Ingawa anaipenda sana biashara yake ya kwanza ya kutengeneza Juisi, anasema kuwa biashara hiyo haina faida kubwa na gharama zake ni za juu sana mbali na kodi inayotozwa.

Tangu ageukie shughuli za kilimo pato limeongezeka na ndio maana amezingatia zaidi biashara hii,kodi inayotozwa katika sekta ya kilimo nchini Uganda ni ya kiwango cha wastani. Lakini nini kilichomchichea kuingilia sekta hii ya kilimo?

**9. Clip Julian 3**

*Niliamua kiingilia shughuli za kilimo kwasababu sikutaka kuwaona watoto wangu wakiomba omba. Nasikia vibaya sana kuona, mtoto eti akitamani matunda mfano Embe unashindwa kumpa kwasababu ya uvivu wako tu wa kukuza mazao hayo na kutegemea zaidi mazao yanayouzwa sokoni. Ukiwa na mazoea ya kununu kila kitu kutoka sokoni, utaweza kuweka akiba ya pesa zako kweli? Pia sikutaka kumuona Mume wangu akinunua chakula kila siku.*

**10. Narrator**

Ingawa sasa anajisimamia, Ufanisi wake anasema unatokana na uungwaji mkono na familia yake.

**11. Clip Julian 4**

*Mume wangu ananisaidia sana. Yeye amesoma kuniliko lakini sii mtu mwenye wivu kama wanaume wengine wanawaonea wivu wake zao wanapokuwa na pesa zaidi kuwaliko. Yeye husema kuwa ‘hata panya anone vipi, bado ni chakula cha paka tu’.*

**12. Short music break**

**13. SFX: Atmo of men loading a lorry with cartons of Cheers juice**

Tunawasili katika kampuni ya Julian ya kutengeneza juisi ya“Delight Uganda”. Hapa tunakutana na wafanyi kazi wanaopakia kinywaji hicho kwenye katoni na kisha kwenye gari kupelekwa sokoni, huku Mumewe Julian akisimamia shughuli hii ya upakiaji wa Juisi aina ya Cheers. Mumewe Felix Omalla anafanya kazi katika idara ya mahakama nchini Uganda na mara nyingi humsaidia Mkewe kufanya kazi katika kampuni yao. Yeye hufurahia sana ufanisi wa Mkewe ingawa mara nyingi inakuwa vigumu kukubali kwamba Mkewe amechukua jukumu la kuwa kiongozi wa nyumba yao. Na katika hali ya kujiliwaza, akabuni sera za kumtambua kiongozi wa nyumba yao.

**14. Clip Felix Omalla**

*Si rahisi kuishi na Mwanamke ambaye anauwezo zaidi wa kifedha kukuliko. Wanawake hupenda sana kuwatongoza wanaume wenye pesa lakini pia mara nyingine Wanaume nao hutaka kuwa na wanawake ambao ni matajiri. Unapomuoa Mwanamke tajiri, lazima ufahamu kwamba si yeye ambaye ni tajiri, bali utajiri huo unatokana na msingi thabiti na muongozo bora wa mumewe, kwahivyo unauwezo zaidi kuliko mwanamke huyo. Yeye ni Mkurugenzi mkuu wa bishara yetu na Mimi ndiye mkurugenzi mkuu wa mkurugenzi mkuu wa kampuni hii yetu laughter).*

**15. Narrator**

Lakini hilo halimjalishi Julian, muhimu ni ufanisi. Yeye hajali tena nani kiongozi wa familia yao kwani anachozingatia zaidi ni ufanisi wa biashara yake. Miaka 15 tangu anzishe biashara hiyo, Julian amaweza kuwaajiri wafanyi kazi 450 kutoka nchini Uganda na Sudan Kusini. Na juhudi hizi zilimfanya kutambulikana kote, na mnamo mwaka wa 2010, Julian alipokea tuzo la kuwa mwanamke bora aliyeweza kubuni nyingi za kazi.

Anakiri kuwa kusimamia kampuni sita si jambo rahisi hasa kwa Mwanamke Barani Africa, ambako kumekuwa na dhana kwamba Mwanamke ni Mtu wa kushughulikia malezi Nyumba. Mbali na hayo Julian hutoa mafunzo kwa kundi la wanawake ambao sasa wanamsaidia kusimamia biashara yake wakiwa na lengo moja la kumpa uwezo na kutambuliwa kwa Mwanamke barani Africa anasema Julian..

**16. Clip Julian 5**

*Mimi najaribu kuwashirikisha na kuwapa mafunzo wanawake zaidi katika shughuli zangu ili nao waweze kujisimamia badala ya kuwategemea waume zao.. Ni lazima sisi wanawake tusaidiane..*

**17. Clip Julian 6**

*Juhudi zetu ndizo zitadhihirisha uwezo wetu kama wanawake. Mimi si mtu wa maneno mengi kwani kila ninapo amka asubuhi nafahamu jukumu langu na hiyo huwa changamoto kubwa kwa wanaume wengi.*

**18. Narrator**

Anasema kuwa kama ilivyo kwa wafanya kazi wengi barani Africa yeye hatumii faida yake yote kuwekeza, bali hutumia sehemu ya pato lake kuwasaidia wasiobahatika miongoni mwa jamii, hasa majirani, jamaa na marafiki. Na hili ndilo jambo linalompa faraja, kwani anaamini kuwa kutoa ni moyo na huleta Baraka katika biashara yake. Anasema kuwa Watu anaowasaidia ndio chanzo cha Baraka kwa kila unachofanya.

**19. Clip Julian 7**

*Hapa barani Africa, Jamaa na marafiki wanahaki ya kula, kunya na kuvaa vizuri,na ni jukumu lako kuwasaidia ukiwa na uwezo huo. Kwa upande wa elimu pia najaribu kuwasaidia, Najaribu sana kushirikiana nao. Mimi ni Mkristo na kila jambo ninalo fanya naamini kuwa ni Baraka kwa wengine, hivyo najaribu sana kuwasaidia hata Mayatima kadri ya uwezo wangu. Ningekuwa nimepiga hatua kubwa kuliko nilivyo sasa lakini pia lazima niwafikirie wengine ambao hawajabahatika maishani..*

**20. Narrator**

Na iwapo unapanga kuanzisha biashara Julian anaushauri wa busara.

## 21. Clip Julian 8

*Kwanza kabisa lazima ufanye biashara ambayo unaielewa vizuri na kujitolea.Lazima utenge muda wa kutosha kwa biashara yako na uipende pia. Ikiwa huna muda wa kusimamia na kutoa muongozo kwa kazi yako kama mmiliki, basi huenda biashara hiyo isifaulu. Lazima uwepo mwenyewe wakati wote.*

*Pili nilazima uweke akiba kwa lengo la kupanua biashara hiyo. Unapasa kuwekeza kutokana na pato la biashara yako na uwe mtu wa subira. Biashara hukua kama binadamu..*

## 22. Narrator

Patricia Bilal ni mshirika wa Julian katika kampuni inayotengeneza Juisi ya Cheers. Yeye anasimamia biashara ya kuoka Mikate mjini wa Juba, Sudan Kusini. Mara kwa mara husafiri hadi nchini Uganda kumtembelea Julian ambaye wameshirikiana kwa muda wa miaka sita sasa. Lakini anamchukuliaje rafiki yake Julian?

## 23. Clip Patricia

*Julian ni mtu mnyenyekevu sana na ndio sababu mimi humpenda. Ni mtu anayependa kazi yake na huwa tayari kukabiliana na changamoto zozote maishani. Mara nyingi huanzisha biashara pasi na kufahamu athari zake lakini baadaye kutokana na mapenzi na juhudi zake, unakuta biashara hiyo inafaulu.*

**24. Narrator**

Kwa kuzingatia jukumu lililombele yake, je Juliana hupata muda wa kuwa na familia yake?

**25. Clip Julian 9**

*Mimi ni bosi wa kazi yangu na inategemea jinsi nitakavyopanga muda wangu baada ya kushauriana na familia yangu. Mume wangu ananisadia sana na nimewafunza watoto wangu kwamba hatuwezi kuwa pamoja wakati wote. Mara yingine hubisha lakini huo ndio ukweli wa mambo.. Na huniuliza, "Mam ,warudi tena Sudan?" na ni lazima niwaeleze sababu zangu za kwenda Sudan na manufaa yake, kisha tunakubaliana.*

**Outro:**

Asante sana Julian Adyeri Omalla kwa hadithi yako ambapo umetufunza mengi jinsi Mwanamke anavyoweza kufaulu kibiashara nchini Uganda. Na hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi cha leo cha Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu wajasirimali chipukizi wanaofaulu na kuchangia katika maendeleo ya jamii wanamoishi. Mwandishi wetu alikuwa Lydia Ndinda. Tunakushukuru wewe msikilizaji kwa kuwa nasi, na iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au kutoa maoni, usisite kutembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine tutakapokutana tena kwa makala nyingine, kwaheri kwa sasa.